

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 27 Juni, 2007

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

TANZIA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninao wajibu mzito asubuhi hii kuwaarifu juu ya jambo zito ambalo limetokea. Kwa moyo mzito na kwa majonzi makubwa, nawathibitishieni, kwa sababu habari zimekwishaanza kusikika kwamba mwenzetu Amina Chifupa Mpakanjia, amefariki dunia jana.

Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, amefariki jana katika Hospitali ya Lugalo saa 2.43 usiku. Akiwa katika dakika zake za mwisho, baba yake mzazi, mama yake mzazi na mumewe walikuwa pamoja naye.

Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, atazikwa kesho kijijini Lupembe, Wilaya ya Njombe, Mkoa wa Iringa, alasiri. Ofisi yangu pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu inafanya mipango ili kuona namna ya ushiriki wa Waheshimiwa Wabunge katika tukio hili kubwa la majonzi kwetu. Kwa hiyo, nawaomba sasa tusimame kwa dakika moja ili kuweza kumkumbuka Marehemu.

*(Hapa Wabunge walismama kwa dakika moja kwa ajili ya kuomboleza kifo cha
Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia)*

SPIKA: Ahsanteni sana.

Kutokana na tukio hili natoa taarifa sasa kwamba Kamati ya Uongozi na Wajumbe wote na Tume ya Huduma za Bunge, tukutane mara nitakapositisha Shughuli za Bunge kwa asubuhi hii. Niseme tu kwamba matangazo zaidi kuhusu nini kitafuata yatafuata baada ya kikao hicho cha Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge. Kwa sasa naweza kusema tu kwamba tunamwomba Mwenyezi Mungu amuweke

Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, mahali pema peponi na awajalie subira wafiwa.
Amin.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 4.00 asubuhi.

(Saa 03.07 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka Saa 04.00 asubuhi)

(Saa 04.00 asubuhi Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nitoe taarifa ya kikao cha pamoja cha Kamati yetu ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge. Napenda tu niseme kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwemo kwenye kikao. Imeamuliwa kama ifuatavyo.

Kwanza kama nilivytangaza mazishi ni kesho kule kijijini Lupembe, ambapo ni kwa mama yake mzazi saa za alasiri, Wilaya ya Njombe. Sasa leo itabidi baadhi yetu twende tukaungane mkono na familia ya Marehemu wakiwa ndio wafiwa ili twende kuwafariji kwa niaba ya Bunge.

Tumeamua tuwe na uwakilishi ambao utajumuisha makundi yetu mbalimbali yaliomo humu ndani ya Bunge. Kwa hiyo, kutakuwa na uwakilishi wa vyama vyaya siasa, kutakuwa na uwakilishi wa maeneo ya nchi yetu yaani kwa maana ya Bara na Zanzibar. Kutakuwa na uwakilishi wa jinsia. Nasikitika kwa Waheshimiwa Wabunge Wanawake ambao wamepitisha azimio kwamba wote waende, haitawezekana.

Niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge, Bunge linafanya kazi zake kwa kitu kinaitwa *precedence*. Mnapoamua jambo muwe na hakika kwamba likitokea jambo lingine kama hilo mtatenda sawa yaani lazima mfanye hivyo hivyo. Sasa kama tukiruhusu kwamba tunapopata msiba akifariki Mbunge mwanamke basi Wabunge wote wanawake wanakwenda kushiriki sidhani kama hilo tutaliweza, lakini tutakuwa na uwakilishi wa kutosha.

Sasa wafuatao tutaondoka nikiongoza ujumbe huo, imepangwa saa 8.00 mchana huu kwenda Dar es Salaam kwa ndege maalumu ya kukodi. Ni ndege kubwa ambayo itatuchukua sio chini ya Wabunge 30 wa Bunge hili.

Uwakilishi wenyewe majina hatujakamilisha hivi sasa, lakini ni kama ifuatavyo, Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Iringa wa Majimbo na Viti Maalum, Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam wa Majimbo na Viti Maalum. Pamoja na hao tutakuwa na wawakilishi wanne wa Vyama vyaya Upinzani wakiongozwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na tutawatamka hivi punde, Katibu Msaidizi wa *CCM Caucas*, Mheshimiwa Rajab Soud na zaidi ya hao wawakilishi wa Serikali, Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Harith Mwapachu, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Simba na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi. Pamoja na hao watakuwepo Katibu wa Bunge na wasaidizi wawili kwa mambo ya utawala kule.

Tumefanya utaratibu ule wa kawaida wa kupata kiwango fulani cha ubani ili tuweze kwenda na kiwango hicho huko.

Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge tumeamua kwamba baada ya sisi kufika Dar es Salaam na kukaa na wafiwa, kuwafariji, kesho ujumbe mdogo zaidi usiokuwa na idadi hiyo hiyo ukiongozwa na Mheshimiwa Mohamed Missanga, utaelekea Njombe pamoja na wafiwa kwa ajili ya mazishi. Sasa kesho asubuhi Bunge litaendelea kama kawaida kwa sababu tunasononeka, lakini kazi za nchi lazima ziendelee. Ila leo hatutaendelea tena na shughuli za Bunge kwa kuheshimu na kumuenzi mwenzetu ambaye ametutoka.

Baada ya kusema hayo nilikuwa nadhani sasa orodha iko tayari ningeomba niyasome majina. Waheshimiwa Wabunge naomba niyasome majina kwa sababu inabidi wahusika wajiandae ili saa nane kasoro robo tuweko *Airport*, Dodoma kwa ajili ya kuondoka.

Kiongozi wa msafara ni Spika, Mheshimiwa Samuel Sitta, Waheshimiwa Wabunge wengine ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Harith Mwapachu, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Peter Msolla, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Salim Hemed na Bwana Damian Foka. Jumla ni 32.

Kama kutakuwa na marekebisho yoyote kwa sababu jambo hili ni la dharura na kama kuna Mheshimiwa Mbunge ambaye ana sababu maalumu basi nadhani badala ya kuwa kama na mjadala tunaweza kufikisha jina kwa Katibu wa Bunge, bado tunao muda.

Labda niketi nione kama kuna jambo lolote pengine upande wa Serikali au wengine wowote. Hakuna jambo lolote upande wa Utawala kuna matangazo yoyote?

Nimetamka saa 8.00 mchana naona saa 6.00 mchana ni mapema mno, kwa hiyo saa 8.00 mchana kuondoka. Niseme tu kati yetu hawa tutafanya mkutano pale kwenye msiba. Mheshimiwa Job Ndugai yumo katika orodha.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nataka kukumbusha tu katika makubaliano yetu walikuwepo wawakilishi wa Kamati husika wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Anne Malecela. Nilitaka kukumbusha katika orodha yako hawakutajwa.

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Job Ndugai. Hali yenyewe ndiyo hii kwa hiyo, si ajabu mambo haya kutokea. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Kwa hiyo, wanakamati wameomba kuwa waweze nao kushiriki na wataongozwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama. Tulikuwa hatujapata majina mengine, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela alikuwa kama mlezi wa binti huyu na nilikuwa namtuma mara kwa mara Dar es Salaam rasmi na nadhani ni mmojawapo wa Wabunge wa mwisho kabisa kuweza kumwona Marehemu. Kwa hiyo, yeye kama mlezi pia tunasafiri naye basi nitasubiri majina yale mengine matatu ya Kamati labda Mheshimiwa Jenista Mhagama unawenza kutupatia?

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, nafikiri tulikuwa tumekubaliana ndani ya Kikao cha Kamati ya Uongozi kwamba mimi mwenyewe kama Mwenyekiti wa Kamati nitaondoka rasmi leo na msafara wako, lakini tulikubaliana na Mheshimiwa Anna Lupembe kwa sababu pia anatoka kule ambako Marehemu anatokea. Kwa hiyo, tulikubaliana na yeye awepo katika msafara huo na kwenye nafasi zile za Kamati tulikubaliana tumuongeze mama yetu mlezi wake Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo taratibu ya Kamati yetu.

SPIKA: Ahsante sana. Nimeendelea kupata ushauri hapa Mheshimiwa Hawa Ghasia yumo katika orodha. Nimekumbushwa lakini yumo katika orodha. Mtu muhimu sana mwingine alikuwa karibu sana na familia naye alikuwa pamoja na Mama Anne Kilango Malecela, nilikuwa namtuma huko *Lugalo Hospital*. Pia ni Mheshimiwa Kapteni John Komba ameongezwa. Samahani sana nimemchukua kwa sababu tulikuwa tukiongea hata jana mpaka saa nane za usiku tunafuatilia. Nimemchukua kama ni sehemu tu ya familia, lakini Kapteni John Komba, tutakuwa naye.

Basi nadhani hayo ndiyo matangazo na kwa kuwa hakuna lingine basi sasa naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 04.13 asubuhi Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 28 Juni, 2007 saa tatu asubuhi)*

